# MTU AWEZAJE KUZALIWA TENA?

na Chuck Smith

Akiwa amejificha gizani, kwa uangalifu mkubwa mtu amwendea Yesu wa Nazareti. Mkuu wa Wayahudi, huyu mtu alingoja hadi ufike usiku, kwa maana alikuwa na swali alilotaka kuuliza, swali ambalo hakutaka mtu mwingine asikie. Akisimama kule nyuma, Nikodemo alimwona Yesu akifanya mwujiza moja baada ya mwingine. Alijua ya kwamba hakuna awezaye kuyafanya haya pasipo Mungu kuwa naye. Lakini mwishowe, Yesu alikuwa pekee yake. Sasa ilikuwa ni wakati wa kuuliza swali lake. ”Rabi,” Nikodemo aliaza, Twajua ya kuwa Hu mwalimu, umetoka kwa Mungu, kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya hizi ishara uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.”Yesu kama ilivyokuwa kawaida yake aliendа moja kwa moja kwa lengo. Alijua kile Nikodemo alitaka. Mtu asipozaliwa mara ya pili” akajibu, “Hawezi kuona ufalme wa Mungu.”

Kwa uadilifu wakati huu, Nikodemo aliuliza, “Ni nini unamaanisha, ‘kuzaliwa” tena?”

Hili swali ndilo watu wengi wamekuwa wakiuliza kwa karne nyingi, wanapotafakari maneno ya Yesu. (Yohana 3:3). Inamaanisha nini kuzaliwa tena?

Tazama, Mungu kwa asili aliumba mtu katika vyeo vitatu; roho, nafsi na mwili. Nafsi hutawaliwa na roho na hivyo roho anapotawala, mtu huishi katika ushirika na mapatano na Mungu. Maisha ya mmea upande mwingi ni kimo kimoja. Ukiwa na mwili asili, hupata chakula chake kutoka kwa mchanga na kwa anga. Mizizi hushikilia mimea isianguke na kuzaana huzanyika kwa utaratibu ndani ya mbegu. Maisha ya mnyama yana pande mbili, mwili upande mmoja na upande mwingine ni “akili”. Wanyama hula mimea au wanyama wengine na hutembea sana. Kama mimea, huuzaana kupitia kwa mbegu yao ya asili ambayo mara kwa mara hutiwa rutuba na mme. lakini kwa sababu ya ufahamu wa nafsini na kuzunguka kwingi, himaya ya wanyama ni ya hali ya juu ukilinganisha na himaya ya mimea.

Sasa, wakati Mungu aliumba mwanadamu, alimwumba katika vyeo vitatu, yaani, akiwa na sehemu tatu, roho, mwili na nafsi. Sehemu ya roho humfanya mwanadamu ainiuliwe juu Zaidi ya himaya ya wanyama, kwa sababu humpa mwanadamu mawasiliano na Mungu.

Yesu alisema Mungu ni Roho na wale wanaomwabudu, lazima wamwabudu katika Roho na kweli (Yohana 4:24). Kwa hivyo mwanzo alipomwumba mwanadamu (na roho, nafsi na mwili), Mungu alimbuni kwa kusudi la ushirika.

Tuna huo msitari wa kupendeza katika Mwanzo 3:8, ”Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu akitembea bustanini wakati wa jua kupunga. ”Mwanadamu alikutana na Mungu na aliishi katika ushirika naye kwa sababu ya sehemu ya roho ndani yake. Ingawaje, roho yake mwanadamu inapokufa, hadhi yake hushushwa hadi kiwango cha hayawani. Shina la fikira zake huwa na msingi katika mahitaji ya kimwili na tamaa zake.

Roho ya mwanadamu imekufa kwa sababu ya uasi na dhambi.

Hapo mwanzo, Mungu alipoumba mwanadamu aliishi katika mzingara kamili na safi. Alikuwa na mwili wenye nguvu, afya usiyo na kasoro ya kizazi, na kwa vile roho yake iliishi, alikuwa na

ushirika na uhusiano na Mungu. Lakini kulikuwa na kasoro. Je, mwanadamu aliishi katika ushirika na Mungu kwa maana alimpenda, au aliishi katika ushirika kwa sababu hakuwa na namna nyingine? Kudhihirisha moyo wa mwanadamu kamili, Mungu aliweka mti wa kupendeza kupindukia katikati ya bustani ya Edeni, mti wenye tunda ambalo lilikuwa la tisho la kifo cha kiroho.

Mwanadamu sasa ilimpasa afanye uamuzi. Je alitaka kuendelea kuwa na ushirika na Mungu au alitaka kutosheleza tamaa zake za kimwili kwa gharama ya kutengana na Mungu?

Kwa bahati mbaya, Adamu alichagua kufuata tamaa ya mwili na akala tunda lilokatazwa. Na kwa kufanya hivyo roho yake ilikufa. Na wakati huo mwanadamu akawa kiumbe chenye sehemu mbili: mwili (asili) na nafsi.

Yesu ngu, lakini tunatakiwa tuzaliwe tena kiroho ikiwa tunatakiwa kujua baraka na furaha iliyo a Mungu. Adamu, akisha iwua roho, aligundua kwamba hapana njia ya kuihuisha kwa kuwa mzuri, kwa kufuata dini au kwa kutimiza sheria na maagizo.

Tunaweza kujaribu kuwa wazuri, lakini hatuwezi kuwa wazuri wa kutosha.

Yesu aliendelea kuongea na Nikodemo, "Mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi kuona ufalme wa Mungu" (Yohana 3:3).

Mtu asili hawezi kuelewa cheo hiki. Hana ufahamu. Paulo aliwaandikia Wakorintho, "Maana ni nani katika binadamu ajuaye mambo ya binadamu ila roho ya mwanadamu iliyo ndani yake? Vivyo hivyo na mambo ya Mungu hakuna ayafahamuye mambo ya Mungu ila Roho wa Mungu. Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia bali Roho itokayo kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. Nayo twayanena si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni. Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu, maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni" ( 1 Wakorintho 2:11-14).

Vile Paulo alivyosema, ndivyo ilivyo kwamba mtu asili hawezi kujua au kuyaelewa mambo ya roho. Ni upuzi kwake. Hii hufanya kuwa vigumu kwetu kuwasiliana kwa sababu kuna bonde kati ya mtu anayetawaliwa na roho na yule anayetawaliwa na mwili.

Je, umewahi kugundua jinsi ilivyovigumu kumweleza mtoto mambo? Inaudhi kwa sababu unafikiri "Kwa nini haelewi? Ijapokuwa inaeleweka. Ni dhahiri. Ni wazi na ya busara. Kwa nini haoni?"

Katika mambo ya kiroho mtu asili ni kama mtoto. Biblia inatwambia kwamba mtu asili hawezi kuyajua mambo ya kiroho kwa sababu yanahitaji ubambanuzi wa kiroho. Ndiyo maana Yesu alisema, "yampasa mtu kuzaliwe mara ya pili kama anataka kuona ufalme wa Mungu" i.

Kwa hivyo swali la Nikodemo lilikuwa wazi, "Ninawezaje kuzaliwa tena? Ni jinsi gani mtu huzaliwa tena? Yawezekanaje mambo haya?" Yesu aliyaeleza akiutumia mfano ambao Nikodemo angeelewa. Alieleza mfano kutoka katika Agano la kale kitabu cha Hesabu. "Watu wakamnung'unikia Mungu, na Musa, mmbona mmetupandisha huku kutoka nchi yaMisri ili tufe jangwani? maana hapana chakula, hapana maji, na roho zetu zinakinai chakula hiki dhaifu" (Hesabu 21:5). Kwa sababu walinung'unika na kulalamika dhidi ya Mungu, aliruhusu nyoka wenye sumu kuingia kambini mwao. Muda si muda mamia ya watu walikuwa wanakufa kwa ajili ya kumwa na nyoka. Waisraeli walimkimbilia Musa na kuomba msamaha, wakimsihi awaombee. Musa naye alimwuliza Mungu kuwaponya watu.

Hata hivyo badala ya kuwaponya, Mungu aliwawekea sharti ambalo lilifanya uponyaji kuwa juu yao. Katika Hesabu 21:8 tunasoma," Bwana akamwambia Musa, jifanyie nyoka ya shaba, ukaiweke juu ya mti na itakuwa kila mtu aliyeumwa aitazamapo ataishi."

Kwa hivyo Musa alijifanyia nyoka ya shaba na akaiweka juu ya mti katikati mwa kambi. Halafu kila aliyeumwa na moja wa hawa nyoka wenye sumu, aliagizwa kuitazama nyoka ya shaba mtini na waliponywa hapo hapo. Hebu nieleze mfano huu maana yake.

Katika maandishi shaba ni mfano wa hukumu ya Mungu. Waisraeli walikuwa na madhabahu ya shaba mahali ambapo dhabihu zao ziliwekwa (2 Wafalme16:15). Pia katika maandishi, nyoka ni ishara ya dhambi (Kumbuka nyoka katika bustani ya Edeni- Mwanzo 3:13).

Hata hivyo, katika kisa hiki, kuinua nyoka juu ya mti ilimaanisha msalaba ambapo Yesu angesulubishwa. Yesu alisema, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa (Yohana 3:14). Na tena Yohana 12:32 alisema, "Nami nikiinuliwa juu ya nchi nitavuta wote kwangu". Yesu alikuwa anatabiri ya kuwa angekufa msalabani.

Kwa hivyo, nyoka wa shaba kwa mti ni mfano wa dhambi zetu zikihukumiwa na Mungu kwa msalaba. Kama vile Musa alivyomwiinua nyoka jangwani, hivyo Mwana wa Adamu sharti ainuliwe. Je mtu awezaje kuzaliwa tena? Anaweza kuzaliwa tena kwa utaratibu ambao Mungu ameweka kupitia kwa kifo cha Mwanawe. Yesu alichukua hukumu ya dhambi zetu juu yake alipokufa badala yetu. Tunapoelewa hili na kumwona Yesu kwa imani pale msalabani, tunagundua ya kwamba alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, akaibeba hukumu ya Mungu ambayo ilikuwa yetu. Hebu fikiria kwamba uliishi na Wana waisraeli karibu miaka elfu tatu iliyopita wakati hawa nyoka walikuja kambini. Siku moja ukiwa unaongea na rafiki yako hemani nyoka ananyinyirika ndani na kumwuma mguuni. Unakosa la kufanya huku mguu wake ukifura halafu baadaye anazimia.

Hivyo unamburura nje ya hema na kulia kwa sauti, "Agalia yule nyoka juu ya mti, yule ambaye Musa alisimamisha katikati ya kambi!" "Sielewi hayo yatanisaidiaaje", anajibu. "Usibishane," unaongea kwa sauti. "Wewe angalia". "Lakini sielewi. Ni vipi kuangalia nyoka aliye juu ya mti kutanisaidia? Mimi nakufa". "Sijui vile itafanyika", unajaribu kumweleza kwa haraka. "Ninajua tu ya kwamba mamia ya watu karibu nasi walikuwa wakifa tu kama wewe, walimtazama yule nyoka juu ya mti na sasa wamepona. Angalia." "Huo tu ni upumbavu," rafiki yako anakataa.

“Mimi sitaangalia.” Halafu rafiki yako anafariki. Na hauwezi kuamimini. Haukumwuliza kufanya kitu kiovu bali ulimwambia tu atazame. Hakuhitaji kuelewa jinsi itakavyofanyika ndipo aweze kufaidika. Vivyo hivyo, Yesu Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, lakini hatutakiwi kuelewa utaratibu wa roho kuzaliwa. Hatutakiwi kujua asili ya mabadiliko, tunachostahili kujua tu ni kwamba inawezekana. Kama Waisraeli jangwani, hatustahili kuelewa taratibu ndipo tufaidike na matokeo. Tunaweza kuishi na fahamu ya nafsini na kushiriki na Mungu. Tunaweza kujua furaha iliyoko katika kuwa na uzima wa milelie na kuwa huru kutoka kwa dhambi.

Yesu alieleza taratibu ya kuzaliwa tena aliposema, Na kama vile Musa alivyomwiinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa: ili kila mtu amwam iniye awena uzima wa milele katika yeye (Yohana 3:14-15). Hakika bila kuzaliwa kiroho wewe unabakia thuluthi mbili ya utimilifu wa mtu. Mtu asili anafahamu ya kwamba kuna kitu ambacho anakosa maishani mwake, na anjaribu mara kwa mara kujaza hilo pengo; shida ni kwamba anataka kujaza hilo pengo na hisia za kimwili ama ujuzi. Lakini baadaye, ingawaje mtu anaweza kuzungukwa na starehe za kimwili ama hisia za ujuzi, bado anapatwa na fikira kwamba kuna kitu kinakosa. Kwa maana hakuna chenye kinaweza kujaza pengo la roho, ila kuzaliwa mara ya pili. Mtu aliumbwa kumwabudu Mungu. Usipomwabudu Mungu wa ukweli na Mungu aishiye, pale utapata badala yake. Inaweza kuwa gari lako, boma lako ama mashua yako. Orodha hii inaweza kuendelea milele. Lakini kuabudu ni tabia ya maumbile yetu kama wanadamu.

Unaweza ukafikiria hii yote ni rahisi. Hauwezi kuelewa jinsi utazaliwa kiroho kwa kumwamini Yesu Kristo. Rahisi vile ilivyo, Mungu aliifanya hivyo ili hata mtoto angeweza kuzaliwa tena mara ya pili. Yesu aliendelea kumwelezea Nikodemo ya kwamba Mungu aliupenda ulimwengu, ulimwengu ambao ulikuwa unaangamizwa na dhambi na kupotea kwa sababu ya dhambi ya kwamba yeyote amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa milele (Yohana 3:16). Nafikiria tena juu ya Waisraeli walipokuwa wakizunguka jangwani, wakimlaumu Mungu kwa shida zao zote, wakinung’unika na kulalamika juu yake kwa sababu ya mateso yao, ili hali ukweli ni kwamba ni wao wakulaumiwa. Na hii ndiyo kawaida ya wanadamu. Tunampa Mungu migongo, tunaishi kimwili. Tunaanza kuona mateso ya maisha ya kimwili – utupu, kuvunjwa moyo, na matokeo yengineyo. Maisha ya kimwili ni mauti. Kama nyoka wa sumu, itakungamiza na utapotea.

Walakini mateso ya muda mrefu ya Waisraeli jangwani haukuwa mpango asili wa Mungu. Alitaka kuwaleta katika nchi ya ahadi, ambapo wangefurahia rotuba, na baraka za nchi; baraka ambazo alikuwa amemwahidi baba yao, Ibrahimu. Lakini walikataa ushuhuda wa Kalebu na Yoshua. Walisema, ”Hatuwezi kupanda tupigane na watu hawa; kwa maana wana nguvu kuliko sisi”. Badala yake waligeuka na kurudi jangwani. Na hapo badaaye, walijaribu kumlaumu Mungu walipo yapata mateso ya kuishi jangwani. Kama unaishi jangwani leo, si kwamba Mungu anataka uishi hapo. Mungu hataki uishi maisha ya kimwili. Anataka uishi maisha kamili ya kiroho, na ufurahie baraka na manufaa yatokanayo kwa kuwa na ushirika naye. Waisraeli walikosa kuelewa kusudi la Mungu, na kwa nini alituma nyoka wenye sumu. Alitaka kuwarejesha kwake. Waona, Mungu mara nyingi ataruhusu mateso kutujia tunapozunguka kwenye maeneo hatari. Anajua tukipitia kenye machungu yatatuamsha, tutamgeukia. Hakika hii si hukumu ya Mungu.badala yake anasema “Njooni kwangu. Hauwezi kuishi bila mimi.

Utaangamizwa. Hapa kuna mfano wa uharibifu unaokuja unapojaribu kuishi bila mimi.” Yote imeundwa kukuleta wewe kwake, kwamba ukaweze kuzaliwa kiroho na kuishi haya maisha ya ajabu ya ushirika na Mungu. Bila usaidizi wa Mungu, Waisraeli wangefariki jangwani. Hawangeishi kwa wiki mbili, chache sana ukilinganisha na miaka arobaini. Vivyo hivyo, Mungu anakuhifadhi hata kama unapita katika jangwa sasa. Bila mkono wa Mungu kukuhifadhi haungemaliza sekundi tano.

Kuishi kwako ni juu yake. Anakuhifadhi ili siku moja uweze kutambua mapenzi yake makuu na haja na utunzi wake juu yako, ili ukaweze kuzaliwa kiroho na kuingia katika mipango yake kamili ambayo Mungu amekusudia kwa kila mmoja wetu. Hivi sasa wengi wenu mnaifuata njia hatari, ambayo inaelekea katika maangamizo. Mnatakiwa kumgeukia Mungu kabla ya kuangamizwa. Ahadi ya ajabu ya Mungu ni kwamba kama tu utamwamini Mwanawe, hautaangamia bali utakuwa na uzima wa milele. Uzima wa milele si kiazi tu. Pia ni ya hali ya juu. Waona kingi bila ubora ni jehanamu. Lakini maisha katika roho yana maisha ya hali ya juu kuliko ya mnyama (au kimwili) usawa wake walinganishwa na kuishi zaidi ya fikira zetu. Na hayo ndiyo maisha ambayo Mungu anakuitia, maisha ya kiroho, maisha ya ushirika naye. Biblia inasema ya kwamba fikira za kimwili ni kifo, lakini fikira za roho ni uzima, amani na furaha. Hayo ndiyo Mungu anatamani upate; uzima wa milele, maisha na furaha, furaha itokayo kwa kuishi katika ushirika na Mungu, ukijua yupo hapo na wewe, akikuelekeza ukijua ya kwamba Mungu anatawala. Mtu huzaliwa kwa kuamini katika toleo la furaha ambalo Mungu alitoa kwa ondoleo la dhambi zako, dhambi ambzo Yesu alibeba mwenyewe. Kwa hivyo ukimpokea Yesu kama mwokozi wako na uamini ya kwamba alikufa kwa ajili ya dhambi zako, kuna mabadiliko ya ajabu yasiyoeleweka ambayo yanaendelea ndani yako wakati roho yako inapozaliwa. Na ghafula unaishi maisha kamili yenye mpaka mpya ya roho ambayo hukuwahi kufikiria na ambayo hukujua yako. Ni jambo la utukufu na pana kuliko chochote ambacho umewahi kupitia awali, na hata itakuwa vigumu kueleza. Paulo alisema kwamba yale aliyoyaona katika roho yalikuwa ya kustaajabisha sana ambayo haijuzu mwanadamu ayanene (2 Wakorintho 12:4). Hakuna lugha ya kuelezea.

Yesu alisema,”Amin, Amin mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuona ufalme wa Mungu.” Kuingia ufalme wa Mungu, lazima uzaliwe mara ya pili. Mtazame Yesu Kristo, aliye kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zako, na umwamini na upendo wake na hayo mageuzo yatapatikana. Hivyo swali, “Je umezaliwa mara ya pili na roho wa Mungu?” Kama hapana, taratibu ni rahisi. Leo uko katika moja ya hizi kambi mbili; yote inategemea uhusiano wako na Yesu Kristo. Unaweza kuamini na kwa Imani umtazame Yesu, aliyekufa kwa ajili yako msalabani; ama unaweza kuendelea jinsi ulivyo. Ni jambo la kushangaza –kupotea, haustahili kufanya chochote. Endelea tu na yale unayofanya sasa na utaangamia. Lakini ukiutazama msalaba na uamini yule aliye kufa kwa ajili ya dhambi zako, basi zawadi ya bure ya Mungu ni yako----zawadi ya uzima wa milele.

Ombi la mwenye dhambi kama unataka kuwa na uhusiano na Mungu na hakikisho kwamba dhambi zako zimesamehewa, hapo kuna ombi lilopendekezwa----Baba, naja kwako nakiri dhambi zangu na kuomba msamaha wako. Nakushukuru Bwana kwa kuwa umeahidi ya kwamba kama nitakiri dhambi zangu, utakuwa mwaminifu kunisamehe na kunitakasa kutokana na udhalimu. Ninataka kutoka katika dhambi zangu, na kuishi kwa njia ambayo itakufurahisha.

Na kwa hivyo ninahitaji msaada wako, Bwana. Naomba unipe nguvu kupitia kwa roho wako ili niishi kikamilifu. Ninakushukuru ya kwamba Yesu Kristo ulikufa msalabani, kulipa deni la dhambi zangu, halafu ukafufuka kutoka kwa wafu. Ninamkubali sasa kama mwokozi wangu, Bwana wangu na rafiki wangu. Pia ninakushukuru, kwa sababu umesema ya kuwa ye yote ajaye kwako, kwa vyo vyote vile hautamkataa. Asante Bwana kwa kunipa maisha mapya katika Kristo. Ninajiachilia kwako. Nifanye kile ambacho wataka niwe. Katika jina la Yesu Amina.

Nini tena?

Kama umeamua kumkubali Yesu Kristo awe Mwokozi wako, sasa umezaliwa mara ya pili. Hapa kuna vitu vichache ambavyo vitakusaidia ukue kama mkristo.

1. OMBA----maombi ni kama laini ya simu, ambayo huenda moja kwa moja hadi kwa Mungu. Ni muhimu kuchukuwa wakati kuongea naye kila siku, mara nyingi (Wafilipi 4:6).
2. SOMA BIBLIA-----Biblia ni kama barua ya upendo kutoka kwa Mungu. Kadiri unavyosoma ndivyo kadiri utakavyompenda hata zaidi (1 Petro 2:2).
3. USHIRIKA----Unatakiwa kuwa na marafiki wenye Imani moja na yako na ambao wanaweza kukutia moyo. Ndiyo maana ni muhimu sana kupata kanisa nzuri ambalo linaamini Biblia ambapo unaweza kupata wakristo wengine (Waebrania 10:24-25).
4. SHUHUDIA KWA WENGINE----shiriki Imani yako katika Yesu Kristo na wengine. Omba kwamba Bwana akufunulie jinsi utashudia na lini (Marko 16:15).

Kama unahitaji usaidizi katika kupata kanisa mahali unaishi, kuwa huru kupiga simu Calvary Chapel Costa Mesa, California. Watumishi wetu wanaweza kukusaidia katika kupata mahali pazuri pakushiriki. Nambari yetu ya simu (714) 979-4422 na tunapatikana saa 9:00 am na 5:00 pm

Pia hapa kuna anwani ambazo zitakusaidia

www.calvarychapel.com\ gospel

www.calvarychapel.com/costamesa/

newbelievers/study/index.htm

www.twft.com

www.calvarychapel.com

Mungu akubiriki na ni ombi letu kwamba utaendelea kuwa karibu na Mungu kila siku!

Chuch Smith, Muhubiri Mkuu Calvary Chapel

Costa Mesa Carlifornia, amekuwa mwalimu wa Biblia kwa zaidi ya miaka hamsini. Mafundisho yake ya Biblia yanaweza kusikika katikati ya wiki kotekote kwa orodha ya redio,

Nen la leo, Baadhi ya vitabu vyake ni “Maji ya Uzima”

“Kwa nini neema hubadilisha kila kitu” na

“Maish ya kufaa ya maombi”

Neno la Leo

S. L. P 800, Costa Mesa, CA

92628

(800) 272-NENO (9673)

www.twft.com

KUZALIWA TENA

Ni Kifungu ambacho tumewahi kusikia

Lakini unajua ukweli maana yake?

Na ni kwa nini Yesu alisema ni lazima kuzaliwa tena kama unataka kuuona ufalme wa Mungu? Hiki kitabu kinaeleza tofauti kati kuzaliwa kimwili na kuzaliwa kiroho.

Na kwa nini Mungu alimwumba mwanadamu

Kwa sababu mwisho si juu ya dini. Ni juu ya uhusiano.